



ONDOLEO LA DHIMA LA MTUMIZI WA BASI

Tafadhali soma kwa umakini kabla ya kuweka sahihi.

Ikiwa mtoto (watoto) wako atatumia usafiri wa basi kwenda na kutoka shuleni, familia yako pia itapaswa kufanya maamuzi ya namna mtoto (watoto) wako atafika kwenye kituo cha basi kilichopangwa. Kama utapenda mtoto (watoto) wako aweze kutembea kutoka kwenye kituo cha basi kufika nyumbani bila kusindikizwa na uangalizi wa mtu mzima, utapaswa kumaliza kujaza hati hii kwanza na kukubali kufuata masharti yote yaliyomo ndani yake.

Watoto waliopo chekechea au darasa la kwanza HAWATORUHUSIWA kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani bila kusindikizwa na mtu mzima, ISIPOKUWA pale watakaposindikizwa na ndugu (ama mtoto mwingine ambaye wewe ni mzazi/mlezi halali kwake), ambaye pia ni mwanafunzi wa Rocketship, aliye darasa la pili, tatu, au nne. Kama mtoto wako yuko chekechea au darasa la kwanza na hauna mtoto mwingine anayesoma darasa la pili, tatu, au nne kwenye shule hiyo hiyo ya Rocketship, mtoto wako hatostahili kutembea kutoka kwenye kituo cha basi bila kusindikizwa na mtu mzima.

Nimeelewa na kukubali kwamba, kwa kuweka sahihi katika hati hii, Ninamruhusu mtoto (watoto) afuataye, **ambaye mimi ni mzazi/mlezi halali kwake**, kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani, au kwenda kwenye kituo rasmi cha matunzo baada ya shule, bila kuwa na uangalizi wa mtu mzima.

Jina la Mtoto: _____ Tarehe ya Kuzaliwa: _____ Darasa: _____

Jina la Mtoto: _____ Tarehe ya Kuzaliwa: _____ Darasa: _____

Jina la Mtoto: _____ Tarehe ya Kuzaliwa: _____

Darasa: _____

(Ongeza nyongeza ya watoto hapa chini au kwenye ukurasa wa nyuma wa hati hii, ikiwa itahitajika)



Ninaelewa kwamba, kwa madhumuni ya hati hii, “mtu mzima” inamaanisha mtu aliye na umri wa miaka 18 au zaidi. Ikiwa nitapenda mtoto wangu asindikizwe na mtu **mwenye umri wa kati ya miaka 11 na 18**, Ninaelewa kwamba nitapaswa kujaza fomu stahiki ya **Makubaliano ya Kukabidhi Mtoto kwa Mtu Mchanga na Ondoleo la Dhima**.

Ninaelewa kwamba, kwa madhumuni ya hati hii, “nyumbani” inamaanisha anuani ya nyumba ambayo nimetoa kwa Rocketship kama sehemu ya nakala zangu za usajili, au mahali pa kituo cha mtoa huduma ya matunzo baada ya shule ambacho nimekitoa kwa Rocketship.

Ninaelewa na kukubali kwamba mtoto yoyote aliyeorodheshwa hapo juu ambaye yupo chekechea au darasa la kwanza HATORUHUSIWA kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani isipokuwa pale atakaposindikizwa na ndugu (au mtoto mwingine ambaye wewe ni mzazi/mlezi halali kwake) ambaye pia ameorodheshwa hapo juu. **Ikiwa mwanafunzi huyo mwenye umri mkubwa hayupo kituo cha basi mwishoni mwa siku, Ninaelewa kwamba ni wajibu wangu, kama mzazi/mlezi, kuweka mpango wa mtu mzima kumchukua mwanafunzi mwenye umri mdogo kutoka kwenye kituo cha basi. Ikiwa mtu mzima hatokuwepo kwenye kituo cha basi kumchukua mwanafunzi, basi mwanafunzi huyo atarudishwa shuleni.**

Ninaelewa na kukubali kuitaarifu shule upesi kama, katika wakati wowote, Nitataka kuongeza au kuondoa mtoto, ambaye mimi ni mzazi/mlezi halali kwake, kuingia au kutoka kwenye hati hii.

Ninaelewa na kukubali kwamba Rocketship **haina wajibu wa kufuatilia tabia za wanafunzi** mara baada ya kutoka kwenye basi, hii ni pamoja na katika kipindi cha kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani.

Ninatambua na kukubali hatari zozote na zote kwa mtoto (watoto) wangu zitakazotokana na kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani bila ya uangalizi wa mtu mzima. Kwa kuzingatia ruhusa ya mtoto (watoto) wangu kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani bila kusindikizwa na mtu mzima, Ninaachilia, naondoa, na kuweka usalama kwa dereva wa basi, mtoa huduma ya usafiri, pamoja na Shule za Umma za Rocketship, na Bodi yake ya Wakurugenzi, maofisa, waajiriwa, watoa huduma ya kujitolea, wakala, wadhamini, wadau au wajumbe, kutoka dhima yoyote na zote, kwangu, mtoto (watoto) wangu, mwakilishi wetu binafsi, wajumbe, wajumbe, na ndugu wa karibu wa majeraha yoyote na yote, madai, madhara, haki za kuchukua hatua au sababu za kuchukua hatua, ambazo Mimi au mtoto (watoto) wangu anaweza kuwa nazo au kupata, kutokana na mtoto (watoto) wangu kutembea kutoka kituo cha basi kwenda nyumbani bila ya kusindikizwa na mtu mzima.

Kwa umakini nimesoma makubaliano haya na nimeelewa maudhui yake. Ninatambua kuwa hii ni hati na ondoleo la dhima, na kwa hiari Ninaweka sahihi.

Ichapishwe na Mzazi/Mlezi

Jina _____



Anuani _____

Namba za
Simu _____
—

SAHIHI _____ Tarehe: _____
